

Jinsi ya kumpa Mtoto Matone ya Vitaminini A na Dawa ya Minyoo

Hatua ya Kwanza: Kabla ya kuanza

Nawa mikono kwa kutumia sabuni na maji

Hatua ya Pili: Jinsi ya kupata taarifa muhimu kutoka kwa mlezi

Uliza umri wa mtoto ili kuamua dozi ya Vitaminini A inayomfaa (miezi 6 hadi 59) na kujua kama mtoto ana umri wa kutosha kupewa dawa ya minyoo.

Hatua ya Tatu: Jinsi ya kumpa mtoto matone ya Vitaminini A

- Hakikisha mtoto ametulia na muombe mlezi wake amshike
- Shika capsule ya Vitaminini A wima, chuchu ikiangalia juu.
- Bado ukishika capsule wima, kata chuchu kwa kutumia mkasi msafi ili kuifungua
- Bonyeza ganda la capsule kuyatoa Matone (ya mafuta) kwenda kwenye kinywa cha mtoto.
- Tupa ganda la capsule lililobaki kwenye ndoo ya taka

Kumbuka:

Kama kituo kitaishiwa matone katika capsules zenyne rangi nyekundu (200,000IU), matone katika capsules mbili zenyne rangi ya bluu (100,000 IU) yanaweza kutumika katika nafasi ya matone katika capsule moja zenyne rangi nyekundu. Kama kituo kitaishiwa matone katika capsules za rangi ya bluu, unaweza kutumia nusu ya matone yaliyomo kwenye capsule ya rangi nyekundu unapomhudumia mtoto aliye kati ya miezi 6 hadi 11.

Hatua ya Nne: Jinsi ya kumpa mtoto dawa ya minyoo

Kwa watoto walio na umri kati ya miezi 12 na 59, mwambie mlezi amwelekeze mtoto atafune na kumeza tembe ya dawa ya minyoo. Kama mtoto hawesi kutafuna, saga kidonge kwa kutumia vijiko viwili au kwa kutumia kijiko na kikombe, ongezeza matone machache ya maji masafi kasha koroga kidogo; kwa msaada wa mlezi, mpe mtoto.

Kumbuka:

Usimlazimishe mtoto kumeza tembe ya dawa ya minyoo kwani kuna hatari kubwa ya mtoto kupaliwa na tembe hiyo. Kama mtoto analia sana au anakataa kumeza tembe, muombe mlezi wake asubiri hadi mtoto atakapotulia na yupo tayari kuimeza.

